

# HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM



## TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA KUKUSANYA USHURU WA MLANGONI NA VYOONI KITUO CHA MABASI UBUNGO

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam anawatangazia wakazi wa Jiji la Dar es Salaam wenye sifa, nafasi ya kazi ya kukusanya ushuru wa mlangoni na vyooni katika kituo cha mabasi Ubungo. Kazi hii itakuwa ni ya Mkataba wa miezi mitatu na mshahara utalipwa kwa kuzingatia Sheria ya Ajira Cap. 300 “Wage Order” 2013 ambao utakuwa kuanzia Sh.150,000/= kwa mwezi.

### SIFA ZA MWOMBAJI:

- Awe Raia wa Tanzania mwenye umri usiopungua miaka 18 na umri usiozidi miaka 60
- Awe na elimu ya darasa la Saba na kuendelea
- Awe na uwezo wa kutumia “Smartphone” katika miamala ya malipo
- Awe na uzoefu usiopungua miezi sita katika masuala ya kukusanya ushuru.
- Awe mwadilifu na mwaminifu na awe hajawahi kutiwa hatiani kwa kosa la jinai

### MAELEKEZO YA JUMLA

- Waombaji waambatishe vivuli vya vyeti vya taaluma zao pamoja na cheti cha kuzaliwa.
- Kila barua ya muombaji iambatishwe na picha mbili ndogo (Passport size) iliyopigwa siku za karibuni, anuani kamili ya makazi pamoja na namba ya simu.

- Barua ya Maombi iambatishwe na:
  - Barua kutoka kwa wadhamini wawili ambao ni watumishi wa Serikali zikiwa na picha “Passport size” ya hivi karibuni, Anuani kamili ya makazi, pamoja na namba zao za simu.
  - Barua ya utambulisho kutoka kwa Mwenyekiti wa Serikali za Mitaa.
  - Wasifu (CV)
- Waombaji watakaokuwa “Shortlisted” watajulishwa kwa njia ya simu tarehe ya usaili.
- Barua ya maombi ya kazi iletwe kwa njia ya mkono katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam kuanzia tarehe ya tangazo hili au kwa njia ya posta kupitia anuani tajwa hapo chini kuanzia saa mbili kamili (2:00) asubuhi hadi saa 8:00 mchana. Mwisho wa kupokea maombi ya kazi ni tarehe 23 Julai, 2018 saa 8:00 mchana.

Maombi yatumwe kwa Anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi wa Jiji,  
Halmashauri ya Jiji,  
Ukumbi wa Jiji,  
1 Barabara ya Morogoro,  
S.L.P. 9084,  
**11882 – DAR ES SALAAM**

Tangazo hili pia linapatikana kwenye tovuti ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ambayo ni **[www.dcc.go.tz](http://www.dcc.go.tz)**



Sipora J. Liana  
**MKURUGENZI WA JIJI**  
**HALMASHAURI YA JIJI LA DAR-ES-SALAAM**